**WIZARA YA AFYA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**JARIDA LA WIKI LA KIEPIDEMIOLOJIA**

*Limetolewa 08/02/2023*

**Wiki ya Kiepidemiolojia ya 05 (30/01/2023 hadi 05/02/ 2023)**


## 1. Utangulizi

Jarida hili limelenga kuwahabarisha wadau wote juu ya mwenendo wa magonjwa, likionesha mambo yafuatayo.

- Milipuko ya magonjwa na matukio yenye athari kiafya yaliyopo nchini na nje ya nchi
- Taarifa za magonjwa yaliyopewa kipaumbele.

## 2. Muhtasari

- Matukio ya **kung'atwa na mnyama nchini - 517**
- **Magonjwa ya mfumo wa njia ya hewa (Sentinel sites)-** Sampuli **227** ambapo sampuli **7 (18.7%)** chanya kwa **Influenza.**
- **UVIKO-19 -** visa vipya **4** kwa kipimo cha **PCR na 45** kwa kipimo cha **RDT** hakuna kifo.
- Surua - Wahisiwa **(21)**
- Homa na vipele (FRI) - **Sampuli 37** ziliwasilishwa maabara
- **Kupooza kwa Ghafla** kuliko Tepetepe (AFP).- **Sampuli 20** ziliwasilishwa maabara
- Kipindupindu - Wahisiwa **wawili (02)** - Halmashauri ya Nyasa
- Kimeta: Mhisiwa **mmoja 1** (Ngorongoro)
- Kichaa chwa Mbwa (Mhisiwa) - (Kifo Manispaa ya Morogoro)



**Kielelezo Na. 1:** Magonjwa ya milipuko yaliyotolewa taarifa wiki ya 05 (Tarehe 30/01/2023 – 05/02/2023), Tanzania Bara

## 3. UFAFANUZI WA KIEPIDEMIOLOJIA TAREHE 30/01/2023 HADI 05/02/2023 (WIKI YA 05)

### 3.1 Hali ya Ugonjwa wa Kipindupindu

Kwa wiki hii wahisiwa wapya wawili (2) wa ugonjwa wa kipindupindu wametolewa taarifa kutoka Halmashauri ya Nyasa Mkoani Ruvuma. Jumla ya wahisiwa 9 na kifo 1 (CFR 11.1%) kilichohusishwa kusababishwa na ugonjwa wa kipindupindu tangu ugonjwa huu utolewe taarifa tarehe 22 Januari, 2023. Mkoa unaendelea ketekeleza afua za kujikinga na maambukizi ya kipindupindu, kutoa elimu mashuleni na kwenye jamii, kushirikiana na sekta nyingine ikiwemo jeshi mpakani ili kuhakikisha wanazuia maambukizi kutoka nchi jirani.

### 3.2 Hali ya Kupooza kwa Ghafla kuliko tepetepe (AFP) wiki ya tano ya kuanzia tarehe 30/01/2023 hadi 05/02/2023


| **HALI YA UGONJWA** | |
|---|---|
| Mfumo wa kielektroniki wa Ufuatiliaji wa Magonjwa yaliyopewa kipaumbele (eIDSR) umepokea taarifa ya mtoto mmoja (1) wa umri chini ya miaka 15 mwenye hali ya Kupooza kwa Ghafla kuliko tepetepe (AFP) kutoka ya Mtwara (Nanyumbu - 1).<br><br>Aidha, Mfumo wa VIMS umepokea taarifa ya Sampuli za watoto 20 wa umri chini ya miaka 15 wenye hali ya Kupooza kwa ghafla kuliko tepetepe (AFP) kutoka Halmashauri 18 katika mikoa 13 | **Hatua zinazoendelea kuchukuliwa**<br>• Kuhimiza mikoa na halmashauri kuendelea kupitia taarifa za wagonjwa katika vituo vya kutolea huduma za afya ili kuibua wahisiwa wa ugonjwa wa Polio.<br>• Kuhimiza mikoa na halmashauri kuendelea kutuma taarifa kupitia mfumo wa eIDSR |

## 3.3 Ugonjwa wa Surua na Rubella (Measles and Rubella) wiki ya tano ya kuanzia tarehe 30/01/2023 hadi 05/02/2023

| HALI YA UGONJWA | |
|---|---|
| Mfumo wa Ufuatiliaji wa Magonjwa yanayozuilika kwa Chanjo (VIMS) umepokea taarifa ya **sampuli 37** za watu wenye dalili za homa na vipere (FRI) kutoka Halmashauri 11<br>✓ Chunya DC-5, Karatu-5, Kiteto-5<br>✓ Bagamoyo-5, Kilolo- 5, Kakonko 5<br>✓ Handeni-2, Ileje-2<br>✓ Njombe TC-1, Temeke MC-1, Kyerwa DC-1 | Aidha, hatua zinazopendekezwa ili kudhibiti mlipuko wa Surua nchini ni:<br>i. Kufanya ufuatiliaji wa watu waliotangamana na wagonjwa pamoja na kutafuta wagonjwa wapya/vifo kwenye jamii na vituo vya kutolea huduma za afya (Active case search)<br>ii. Kutoa elimu juu ya ugonjwa wa Surua na umuhimu wa chanjo kwenye jamii<br>iii. Kutoa matibabu sahihi kwa wagonjwa wote waliopatikana<br>iv. Kufanya kampeni ya uchanjaji kwa watoto wote ambao hawajachanja na waliohasi chanjo<br>v. Utoaji wa matone ya Vitamin A kwa watoto wote waliokuwa wakipatiwa chanjo ya Surua na Rubella na kwa wateja waliokuwa na dalili za surua |

## 3.4 Magonjwa ya Mfumo wa Njia ya Hewa (SARI/ARI/ILI) wiki ya tano ya kuanzia tarehe 30/01/2023 hadi 05/02/2023

| **HALI YA UGONJWA** | |
|---|---|
| Jumla ya wahisiwa 234 wenye dalili za magonjwa mafua makali (SARI) na mafua yasiyo makali walitolewa taarifa<br><br>Jumla ya sampuli 227 za watu wenye mafua maki na mafua yasiyo makali sana (ARI/ILI) kutoka vituo 17 (68%) kati ya 25 vya "Influenza *sentinel Sites"* zilikusanywa na kutumwa maabara ya Taifa kwa vipimo vya Influenza na UVIKO-19.<br><br>Majibu ya sampuli 227 yalikuwa kama ifuatavyo:<br>✓ Sampuli 3 (1%) zilionesha kuwa na virusi vya UVIKO-19 kutoka mikoa ya Dar es salaam -1, Kigoma – 1 na Mtwara -1<br>✓ Sampuli 7(3%) zilionesha uwepo wa Influenza kutoka mikoa ya Manyara -1, Mtwara – 3, Tabora – 1 na Iringa -2. | Aidha, virusi hivi vya mafua ni vya kawaida na siyo vya mlipuko (seasonal influenza)<br><br>Idadi ya sampuli zilizotumwa Maabara ya Taifa zimefikia lengo la Kitaifa ambalo ni angalau sampuli 150 kwa wiki, nchi nzima.<br><br>**Hatua zinazoendelea kuchukuliwa**<br>Kuendelea kusisitiza Sentinel sites kuchunguza wagonjwa wote wanaofika katika vituo vyao ili kuweza kutambua wagonjwa wanaokidhi vigezo vya utambuzi kwa ajili ya kuchukuliwa sampuli. |




**Kielelezo Na. 2:** Mwenendo wa sampuli na majibu ya Chanya ya Influenza na COVID-19 kuanzia wiki ya 40, mwaka 2022 hadi wiki 5 mwaka 2023 (Tarehe 30/01/2022 – 05/02/2023), Tanzania Bara

### 3.5 Matukio ya kung'atwa na wanyama wiki ya tano tarehe 30/01/2023 hadi 05/02/2023

| HALI YA UGONJWA | |
|---|---|
| Jumla ya watu 517 waliong'atwa na wanyama wametolewa taarifa.<br><br>Mikoa iliyokuwa na idadi kubwa ya watu waliong'atwa na wanyama ni<br>✓ Ruvuma – 115,<br>✓ Dodoma – 67,<br>✓ Tanga – 37,<br>✓ Arusha – 32,<br>✓ Kigoma – 26, | Matukio ya waliong'atwa na wanyama kwa wiki hii yameongezeka kwa 16.6% ikilinganishwa na watu 431 waliotolewa taaarifa wiki iliyopita.<br><br>Baada ya kuchakata takwimu za matukio ya kung'atwa na mnyama ilibainika kuwa mikoa mitano Ruvuma, Dodoma, Tanga, Arusha na Kigoma ina idadi kubwa ya matukio hayo |

Mikoa yenye matukio ya kung'atwa na wanyama kwa wiki ya Tano, Mwaka 2023




**Δ** Kung'atwa na Mnyama

Jumla ya matukio 517 kung'atwa na Wanyama bila kifo yametolewa taarifa kwa wiki ya Tano, mwaka 2023.

| Na | Mkoa | Wiki ya 04 | | Wiki ya 05 | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Wagonjwa | Vifo | Wagonjwa | Vifo |
| 1 | Arusha | 38 | 0 | 32 | 0 |
| 2 | Dar Es Salaam | 10 | 0 | 14 | 0 |
| 3 | Dodoma | 20 | 0 | 67 | 0 |
| 4 | Geita | 4 | 0 | 6 | 0 |
| 5 | Iringa | 11 | 0 | 10 | 0 |
| 6 | Kagera | 18 | 0 | 22 | 0 |
| 7 | Katavi | 4 | 0 | 1 | 0 |
| 8 | Kigoma | 12 | 0 | 26 | 0 |
| 9 | Kilimanjaro | 38 | 0 | 20 | 0 |
| 10 | Lindi | 27 | 0 | 12 | 0 |
| 11 | Manyara | 21 | 0 | 10 | 0 |
| 12 | Mara | 6 | 0 | 14 | 0 |
| 13 | Mbeya | 10 | 0 | 19 | 0 |
| 14 | Morogoro | 39 | 0 | 23 | 0 |
| 15 | Mtwara | 4 | 0 | 1 | 0 |
| 16 | Mwanza | 21 | 0 | 19 | 0 |
| 17 | Njombe | 4 | 0 | 2 | 0 |
| 18 | Pwani | 8 | 0 | 11 | 0 |
| 19 | Rukwa | 3 | 0 | 4 | 0 |
| 20 | Ruvuma | 19 | 0 | 115 | 0 |
| 21 | Shinyanga | 6 | 0 | 1 | 0 |
| 22 | Simiyu | 3 | 0 | 8 | 0 |
| 23 | Singida | 70 | 0 | 9 | 0 |
| 24 | Songwe | 1 | 0 | 22 | 0 |
| 25 | Tabora | 18 | 0 | 12 | 0 |
| 26 | Tanga | 16 | 0 | 37 | 0 |
| | **Jumla ya** | **431** | **0** | **517** | **0** |

### 3.6 Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa (Rabies)

Mhisiwa mmoja (01) wa ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa alikuwa amefariki kutoka katika Manispaa ya Morogoro mkoani Morogoro. Wizara imewasiliana na Mkoa na hatua mbalimbali zinaendelea ikiwemo kuchunguza tukio hilo na kuchukua hatua ikiwemo kutoa elimu kwa wananchi, kutafuta watu wengine waliong'atwa na mnyama mwenye kuhisiwa na ugonjwa na uchanjaji kwa wanyama jamii yam bwa na paka.


### 3.7 Ugonjwa wa Kimeta (Anthrax)

| **HALI YA UGONJWA** | |
|---|---|
| Katika wiki hii mhisiwa 1 wa ugonjwa wa Kimeta alitolewa taarifa kutoka Mkoa wa Arusha (Ngorongoro).<br><br>• Aidha, sampuli ilichukuliwa kwa wahisiwa wa ugonjwa wa Kimeta kutoka Ngorongoro na kupimwa katika maabara ya kituo cha kutolewa huduma kwa gram stain na ilionesha kuwa na maambukizi ya ugonjwa wa kimeta<br><br>**Changamoto**<br>• Jamii kuendelea na tabia ya kula wanyama walio kufa.<br>• Uchanjaji hafifu wa wanyama(vacination coverage) kati katika Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro<br>• Kutokutoa taarifa za wahisiwa kwa ukamilifu na wakati kwa kutumia mfumo wa kutolea taarifa (eIDSR). | **Mambo Yaliyofanyika**<br>- Kuendelea kushirikiana na Wizara ya Mifugo kuhakikisha mipango ya uchanjaji wa ng'ombe, mbuzi na kondoo inatekelezwa ipasavyo<br>- Kutoa elimu kwa jamii kwa watu wenye dalili kufika katika vituo vya kutolea huduma na kuendelea kuibua wagonjwa<br>- Kuendelea kuwajengea uwezo wataalam kupitia njia mbali mbali ikiwemo mafunzo kazini na usimamizi shirikishi namna ya kutumia mfumo wa IDSR. |

## 4. Hali ya Utumaji wa taarifa kwenye mfumo wa IDSR kwa Wiki ya tano mwaka, 2023

### 4.1. Uwasilishaji wa taarifa Kimkoa

Katika wiki hii, mwenendo kimkoa wa utumaji taarifa za magonjwa hapa nchini kwa wiki unaonesha kuwa Mikoa 19 (73.1%) ilifikia lengo la kitaifa la utumaji wa taarifa (Completeness >=90%) na kwa wakati (Timeliness >=90%). Ambapo kwa wiki viwango hivi vilikuwa 90.0% na 90.0% kwa mfuatano wa ukamilifu na wakati




**Kielelezo 2**: Mwenendo Kimkoa wa utumaji taarifa za magonjwa *(Diarrhea, Malaria, Pneumonia, Animal bite, Snake bite na Typhoid*) yanayotolewa taarifa kwa wiki hapa nchini kwa wiki ya tano, mwaka 2023.

## Uwasilishaji wa Taarifa za ndani ya saa 24 Kimkoa

### Changamoto

- Kulitokea shida ya kiufundi katika mfumo wa e-IDSR kwa mtandao wa Vodacom na hivyo kuathiri utumaji wa taarifa kwa watumiaji waliosajiliwa na namba za Vodacom. Watalaam wanaendelea kutafuta ufumbuzi wa hili.

### Hatua Zinazochukuliwa

- Wizara imeendelea
  - ✓ kutoa mrejesho kwa Waratibu wa Mikoa kusimamia utumaji wa taarifa kwa ukamilifu na wakati
  - ✓ kushauri vituo kutumia mfumo wa DHIS2 na kutumia mitandao mingine kama Halotel, Tigo, Airtel

## 5. UVIKO-19

### 5.1. Mwenendo wa maambukizi, upimaji na hali ya chanjo ya UVIKO-19 kwa wiki ya tarehe 28/01/2023 – 03/02/2023

Katika wiki hii watu **616** walipimwa kwa kutumia RT PCR na kati yao, watu **4** walithibitika kuwa na maambukizi sawa na **6.7%** ya waliopimwa. Kwa wiki tajwa, hakuna mgonjwa mpya aliyekuwa amelazwa. Watu **3,736** walikuwa wamepimwa kwa vipimo vya haraka (RDTs) katika vituo vya kutolea huduma za afya na kati yao, watu **45** sawa na **1.2%** walikutwa na maambukizi. Tangu mlipuko wa UVIKO-19 uanze nchini hadi tarehe 03 Februari 2023, jumla ya vipimo vya maabara **(RT PCR) 346,590** na **357,190 (RDTs)** vilikuwa vimefanyika. Jumla ya watu waliothibitika kwa **RT PCR ni 37,037 na 4,022** walithibitika kwa **RDTs.** Jumla ya **vifo 808**, sawa na asilimia **2.2% (CFR**) ya waliougua toka mlipuko uanze Machi, 2020 vilikuwa vimetolewa taarifa.

Kwa wiki tajwa jumla ya watu wapya **139,921** walikuwa wamechanjwa chanjo za UVIKO-19. Hivyo, hadi tarehe 03 Februari, 2023 jumla ya watu **31,898,420** walikuwa wamekamilisha dozi za chanjo za UVIKO-19 sawa na asilimia **53.3** ya idadi ya watu Kitaifa ambao ni sawa na asilimia **103.8** ya watu wenye umri wa miaka 18 na zaidi (n=30,740,028).

**Mwenendo wa upimaji wa UVIKO-19 na hali ya chanjo ya UVIKO-19 Tanzania**

| **Viashiria** | **Tarehe** | |
|---|---|---|
| | **21 – 27/1/2023** | **28/1/23 – 3/2/23** |
| Idadi ya vipimo vya PCR | 702 | 616 |
| Idadi ya waliothibitika kwa PCR | **3** | **4** |
| Kiwango cha waliokutwa na maambukizi (Positivity Rate) kati ya waliopimwa kwa PCR | **0.4%** | **0.6%** |
| Idadi ya vipimo vya RDTs | 2,857 | 3,736 |
| Idadi ya waliothibitika kwa RDTs | **57** | **45** |
| Kiwango cha waliokutwa na maambukizi (Positivity Rate) kati ya waliopimwa kwa RDT | **2%** | **1.2%** |
| Jumla ya vipimo vya PCR na RDTs | 3,559 | 4,352 |
| Jumla ya waliothibitika kwa PCR na RDTs | 60 | 49 |
| Kiwango cha waliokutwa na maambukizi (Positivity Rate) kati ya waliopimwa kwa PCR & RDT | **1.7%** | **1.1%** |

## 6. TETESI

Tangu tarehe 01 Januari 2023 hadi 05 Februari 2023 jumla ya tetesi 433 zilikuwa zimepokelewa kutoka mkoa wa Arusha na Kagera ambapo Jumla ya tetezi **145** sawa na **33.5** zilikizi vigezo vya kufanyiwa uchunguzi.